

Tanzania, Mpunga, Ajira Kwa Watoto

Kuna ushahidi kuwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18 wanafanya kazi ya uzalishaji wa mpunga nchini Tanzania. Kutokana na uchambuzi wa Uchunguzi Jumuishi wa Nguvu Kazi Tanzania wa mwaka 2020/21, inakadiriwa kuwa watoto 232,470 walio chini ya umri wa kufanya kazi wanashiriki katika uzalishaji wa mpunga. Watoto wanaofanya kazi katika kilimo huenda wakawa katika mashaka ya kuathiriwa na hatari kadhaa ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa masaa mengi, kubeba mizigo mizito, kutumia zana hatari, kujiweka wazi kwa athari za hali ya hewa, majeraha ya kimwili na kemikali, kama vile viuadudu. Serikali ya Tanzania inapaswa kupongezwa kwa kuendesha na kuchapisha data za uchunguzi zinazosaidia kubuni na kutekeleza sera na programu madhubuti ili kukabiliana na ajira kwa watoto.